Voluntary Assisted Dying
QUEENSLAND

# Kiswahili

## kusaidiwa kufa kwa hiari

Queensland Government

Ikiwa unahitaji mkalimani, Muombe daktari wako mkalimani. Ni bure.

Ili Kupata msaada kusoma habari hii ita:

- Namba ya simu ya (Multicultural Connect Line) utamaduni kwa bure: 1300 079 020
- Huduma ya ukalimani (msaada wa kiingereza): 13 QGOV (13 74 68) alafu omba mkalimani
- Huduma ya kutafsiri na ukalimani: 13 14 50

# Maneno magumu

Kitabu hiki kina baadhi ya maneno magumu.

Tunapo andika neno gumu kwa mara ya kwanza:

- neno hilo liko katika **bluu**
- tunaandika neno hilo gumu linamaanisha nini.

# Kuhusu kitabu hiki

Kitabu hiki kimeandikwa na Queensland Health (Queensland afya).

Kitabu hiki kinahusu **Kusaidiwa Kufa Kwa Hiari.**

*Kusaidiwa Kufa Kwa Hiari inamaanisha, baadhi ya watu wanaweza kuomba msaada ili kukatisha uhai wao. Watu wanaoweza kuomba msaada ili kukatisha uhai wao ni wale tu walio wagonjwa sana na ambao watakufa katika muda wa chini ya miezi 12.*

Hiki kitabu kinaweza kukusaidia kujua, Kusaidiwa kufa kwa hiari ni nini.

Kitabu hiki ni kwa ajili ya watu wanaotaka kujua mengi zaidi kuhusu Kusaidiwa Kufa Kwa Hiari.

**Unaweza pata mtu atakaye kusaidia:**

- soma hiki kitabu
- jua yale ambayo hiki kitabu kinahusu
- tafuta habari zaidi

Baadhi ya watu ambao wana imani tofauti kuhusu kifo na kufa wanaweza kukasirishwa na kusoma hiki kitabu.

# Nini la kufanya ili kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari

*Kutumia ni wakati unaweza kujua jinsi uweza kufa kwa kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari*

Unaweza kuchagua kufanya Kusaidiwa kufa kwa hiari

Omba Kusaidiwa kufa kwa hiari wewe mwenyewe.

Hakuna mtu mwingine ambaye anaweza kuomba Kusaidiwa kufa kwa hiari kwa niaba yako.

Hakuna yeyote anayeweza kukufanya uombe Kusaidiwa kufa kwa hiari.

Unaweza kusitisha Kusaidiwa kufa kwa hiari wakati wowote.



## Daktari wako na Kusaidiwa kufa kwa hiari

Sio lazima Daktari wako akufanyia Kusaidiwa kufa kwa hiari



Ikiwa Daktari wako hakufanyii Kusaidiwa kufa kwa hiari unaweza kuita **Queensland Kusaidiwa kufa kwa hiari huduma ya msaada (QVAD-Msaada)**.

*Queensland Kusaidiwa kufa kwa hiari huduma ya msaada (QVAD-Msaada) inaweza kukusaidia kupata daktari ambaye anafanya Kusaidiwa kufa kwa hiari*

Unaweza kuwasiliana na (QVAD-Msaada)Jumatatu hadi Ijumaa, saa 2 asubuhi - saa 10 jioni (8.30am-4pm)

**Email:** QVADSupport@health.qld.gov.au

**Simu:** 1800 431 371

# Nani anaweza tumia Kusaidiwa kufa kwa hiari



**Unaweza tumia Kusaidiwa kufa kwa hiari ikiwa tu:**

- una ugonjwa ambao utakusababishia kifo katika kipindi cha chini ya miezi 12
- una ugonjwa ambao unakusababishia maumivu makubwa ya kimwili na kiakili ambayo unaona hayavumiliki
- una ugonjwa ambao hauwezi kupona na hautaacha kukusababishia maumivu
- unaweza kujifanyia maamuzi
- unapenda kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari
- una umri wa miaka zaidi ya 18
- unaishi Queensland na ni mkaaji (mkazi)(wa Queensland)

**Hauwezi kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari ikiwa:**

- Una ugonjwa wa akili lakini hauna ugonjwa ambao utakusababishia kifo katika miezi 12 ijayo
- Una ulemavu lakini hauna ugonjwa ambao utakusababishia kifo katika miezi 12 ijayo
- Hauwezi kujifanyia maamuzi
- Hauko mgonjwa

# Mambo ya kufanya ili kupata na kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari

Ili kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari utaiaji kuiomba mara tatu na kuonana na madaktari wa wili.



## Ombi la kwanza

Ombi la kwanza ni wakati unamuomba daktari wako Kusaidiwa kufa kwa hiari

## Tathmini ao uchunguzi wa kwanza



Tathmini ao uchunguzi wa kwanza ni wakati:

- Daktari wako anakuambia ikiwa unaweza ao hauwezi kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari
- Daktari wako atakupa habari za kukusaidia kuamua ikiwa unataka kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari

## Tathmini ya ushauri



Tathmini ya ushauri ni wakati:

- Daktari wako anakuomba umuone daktari mwingine
- Daktari wa pili anakuambia ikiwa anakubaliana kama unaweza kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari

## Ombi la pili



Ombi la pili ni wakati:

- Unaomba Kusaidiwa kufa kwa hiari kwa kuandika
- Daktari wako anakupa fomu ya kufanya hili
- Watu wa wili wanakutazama ukitia saini kwenye fomu.
- Kama hauwezi kutia saini kwenye fomu mtu mwingine anaweza kutilia saini, ikiwa utawaomba.

## Ombi la mwisho



Ombi la mwisho ni wakati:

- Unamuomba daktari wako mara ya tatu Kusaidiwa kufa kwa hiari
- Lazima kuwe angalau siku tisa kati ya ombi lako la kwanza na lile la mwisho Hii ni kukupa muda wa kuakikisha unataka Kusaidiwa kufa kwa hiari
- Unaweza kumuomba Daktari wako kwa kutumia maneno, kuandika maneno ao kuonyesha kwa kutumia mkono ao njia nyingine.

## Mapitiyo ya mwisho



Mapitiyo ya mwisho ni wakati:

- Daktari wako anakuambia ikiwa bado unaweza kutumia Kusaidiwa kufa kwa hiari Daktari wako atachunguza ikiwa mchakato umefanywa ifahavyo

## Uamuzi wa matumizi (kudhibiti)



Uamuzi wa matumizi ni wakati:

- Unafanya chaguo kuhusu jinsi unavyotaka **Dutu ao dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari litakavyo tumiwa**.

  *Dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari ni kidonge kinacho sababisha kifo.*
- Kuna chaguo mbili:
  - Unaweza kuchagua kuitumia dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari wewe mwenyewe
  - Unaweza kuchagua kutumia daktari wako kukupe dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari.
- Daktari wako atazungumza nawe kuhusu changuo lililo bora zaidi kwako.



# Uteuzi wa mtu wa mawasiliano

Ikiwa tayari umefanya uamuzi wa kudhibiti, lazima uchague **mtu wa mawasiliano**.

*Mtu wa mawasiliano ni mtu ambaye anakusaidia kwenye sehemu ya mwisho ya Kusaidiwa kufa kwa hiari Anapaswa kuwa wa umri zaidi ya 18*

Uteuzi wa mtu wa mawasiliano ni wakati:

- Unachagua mtu fulani awe mtu wa mawasiliano. Anaweza kuwa mwenzi wako, mwanafamilia, rafiki, mlezi, mtumishi wa huduma ya afya wala mtu fulani unaye amini.
- Mtu wako wa mawasiliano anamjulisha daktari wako wakati umekufa.
- Ikiwa kuna dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari iliyo baki baada ya wewe kufa, mtu wako wa mawasiliano anairudisha kwenye duka la madawa.



# Kukatisha uhai wako

**Ikiwa umechaguwa kutumia dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari wewe mwenyewe.** Mfamasia kutoka kwenye Queensland Kusaidiwa kufa kwa hiari huduma ya duka la dawa (QVAD-Pharmacy) atakupa dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari ambayo utatumia kukatisha uhai wako.

**Ikiwa umechagua daktari wako ao muuguzi akupe dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari**, daktari wako ao muuguzi atakupa dawa ya kukatisha uhai wako, huku mtu mwingine akitazama.

# Baada ya kufa

## Kutupwa kwa dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari

Kutupwa kwa dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari ni wakati:

- Ikiwa umechagua kudhibiti ao kutumia dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari wewe mwenyewe, mtu wako wa mawasiliano ataitaji kurudisha dawa ao dutu zilizo baki kwenye duka la dawa. Wataambiwa jinsi yakufanya hivyo.
- Ikiwa umechagua daktari ndiye akudhibitie ao kutumia dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari. Daktari wako ao muuguzi atatupa dawa yoyote iliyo baki.

## Taarifa ya kifo



Daktari wako atajulisha baraza la ukaguzi la Kusaidiwa kufa kwa hiari ya kwamba Umekufa.

## Cheti cha kifo

Cheti cha kifo ni karatasi inayosema jinsi umekufa.

Cheti cha kifo kitasema umekufa kutokana na ugonjwa wako (kwa mfano, saratani).

# Kuongea kuhusu Kusaidiwa kufa kwa hiari



Kuongea kuhusu kifo na Kusaidiwa kufa kwa hiari inaweza kuwa gumu na yenye huzuni.

Watu wanataka kuutumia vema wakati waliobaki nao.

Chaguo ambazo watu hufanya ni za kibinafsi sana na muhimu kwao.

Kuongelea kuhusu yale unayo taka uisaidia familia yako na walizi ao wauguzi kuelewa.

Unapo ongelea kuhusu Kusaidiwa kufa kwa hiari, jambo gumu zaidi ni kujua kwa kuanzia

Hapa kuna baadhi ya mawazo:

- "Hili ni gumu kuzungumzia, lakini lina maana sana (kubwa) kwangu."
- "Tumesha zungumzia kuhusu kitakacho tokea baada na mimi kufa. Je, tunaweza zungumzia zaidi kuhusu Kusaidiwa kufa kwa hiari?"
- "Nimekuwa nikiongea na daktari wangu. Daktari aliniomba ni fikirie kuhusu yale ambayo ningetaka kufanya."

# Msaada kwa famili na wahudumu



Baada ya kifo chako familia yako na wahudumu wako wanaweza wakaisi huzuni na asira.

Kuna njia nyingi za wao kupata msaada.

Daktari wako anaweza saidia familia yao na wahudumu kupata msaada unao faa.

Kwa msaada zaidi, wanaweza kuita QVAD-Msaada:

**Email:** QVADSupport@health.qld.gov.au
**Simu:** 1800 431 371

## Baraza la ukaguri la Kusaidiwa kufa kwa hiari ni nini?

Kazi yao ni ku akikisha kila mtu anafuata sheria kuhusu Kusaidiwa kufa kwa hiari.

## QVAD-Msaada ni nini?

Kazi yao ni ku:

- wapa habari na msaada watu wanaotaka Kusaidiwa kufa kwa hiari
- Saidia watu wanaotaka Kusaidiwa kufa kwa hiari
- Unganisha watu na wahudumu wa afya na huduma ambazo zinafanya Kusaidiwa kufa kwa hiari
- Saidia wahudumu wa afya ambao wanafanya Kusaidiwa kufa kwa hiari

## QVAD-Pharmacy ni nini?

Kazi yao ni ku hakikisha dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari inatumiwa kwa usalama na inatupwa ao kuaribiwa kwa usalama.

Wana akikisha daktari ao muuguzi anajua ujinsi ya kutumia dawa ya Kusaidiwa kufa kwa hiari

# Kupata msaada



Baadhi ya watu wanaweza wakaisi huzuri kwa kusoma haya. Kama kusoma haya kume kufanya ao kumefanya mtu fulani kuwa na asira na unaitaji msaada, tafadhali ita moja wapo ya nambari zilizo hapa chini.

- Queensland utamaduni kituo cha afya ya akili ita 3317 1234 ao 1800 188 189 (nje ya Brisbane) ao 1300 64 22 55 (ma saa 24)
- Kundi la afya ya ulimwengu (msaada wa utamaduni) ita 1300 079 020

Kwa habari zaidi na msaada tembelea https://www.qld.gov.au/health/mental-health/help-lines.